

HALMASHAURI YA WILAYA BUSEGA –SIMIYU

SHULE YA SEKONDARI SHIGALA

S L P 301

BUSEGA

KUMB.NA.SHSS/JI/KI/2021/0015

MZAZI/MLEZI WA.....

SHULE YA MSINGI.....

BUSEGA – SIMIYU

YAH.MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SHIGALA KIDATO CHA KWANZA MWAKA.....

1. UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari shigala iliyoko wilaya ya busega mkoa wa simiyu. Shule ya sekondari shigala ni ya kutwa yenye wanafunzi mchanganyiko (wavulana na wasichana) na ipo umbali wa kilometa 15 mashariki mwa halmashauri ya busega .wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe.....

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A.SARE ZA SHULE WAVULANA

- ✓ Suruari 2 rangi ya **blue bahari**-isiwe modo tafadhali
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi visivyokuwa na visigino virefu vyenye kamba
- ✓ Soksi nyeusi
- ✓ Tai ya blue bahari
- ✓ T-shirt ya njano na track suit(suruali) nyekungu
- ✓ Raba nyeusi

B.SARE ZA SHULE WASICHANA

- ✓ Sketi 2 rangi blue bahari mashono ni linda box **iwe ndefu hadi kwenye kisigino**
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi sawa na vya wavulana
- ✓ Soksi nyeusi

- ✓ Tai blue bahari
- ✓ Hijabu rangi ifanane na sare za shule mashono kutegemea na dini husika
- ✓ Track suit ya kijani (suruuri na tshirt)
- ✓ Raba nyeusi

C.VIFAA VYA KUJIFUNZIA PAMOJA NA VYA USAFI

- ✓ Daftari kubwa 10 (counter books)
- ✓ Kalamu za kutosha
- ✓ Rula
- ✓ Mathematical sets 1
- ✓ Dictionary/kamusi
- ✓ Folder file 1
- ✓ Soft bloom 1 kwa wavulana
- ✓ Ndoo ndogo 1 kwa wasichana

3. SHERIA NA KAUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti.

- a. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b. Mahudhurio mazuri ya kila shughuli ndani ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c. Kushiriki kwa makini kujifunza kwa bidii shuleni na nyumbani.
- d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyengine utakazopewa.
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule.
- f. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h. Kuzingatia ratiba ya wakati wote.
- i. Kutunza mali za shule.

4. MAKOSA AMBAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- 1) WIZI
- 2) UASHERATI NA USHOGA
- 3) UBAKAJI
- 4) ULEVI NA MATUMIZI YA MADAWA YA KULEVYA kama vile kuvuta bangi,cocaine,mirungi,kuberi n.k.
- 5) KUPIGANA AU KUPIGA
- 6) KUHARIBU KWA MAKUSUDI MALI YA UMMA
- 7) KUDHARAU BENDERA YA TAIFA
- 8) KUWA MJAMZITO /KUPATA MIMBA
- 9) KUOA AU KUOLEWA
- 10) KUTOA MIMBA
- 11) KUGOMA, KUCHOCHA, KUONGOZA AU KUSHIRIKI KUVURUGA AMANI NA USALAMA WA SHULE AU WATU.
- 12) KUKATAA ADHABU KWA MAKUSUDI
- 13) KUWA NA SIMU YA MKONONI

5. MAMBO MENGINE MUHIMU AMBAYO YANATAKIWA KUKAMILISHWA NA MWANAFUNZI ATAKAPO KUWA ANARIPOTI SHULE.

- Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu hospatali ya serikali .Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.KIAMBATISHO B
- Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai na mzazi /mlezi kukubaliana na sheria ,kanuni na melekezo mengne yatakayotelewa na shule .KIAMBATISHO A NA C

MHIMU

- Soma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu
- Hakikisha unakamilishia mahitaji yote mwanao kabla hujamleta shule
- Sare zote za shule na za michezo aje nazo shuleni siku ya kuripoti ili zikaguliwe

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA SHIGALA SEKONDARI

.....

KIJA M MADUHU

MKUU WA SHULE SHIGALA

0763-015136 / 0620-404681